

SHIRIKA LA MAENDELEO YA PETROLI TANZANIA (TPDC)



TAARIFA KWA UMMA

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC) chini ya Wizara ya Nishati na Madini linapenda kuufahamisha umma kuwa, tarehe 08/03/2017 na tarehe 13/03/2017 imefikia makubaliano na Kampuni ya **Dangote Group of Industries** juu ya bei ya mauziano ya gesi asilia kwa ajili ya matumizi ya kiwanda hicho cha kutengeneza saruji kilichopo Mkoani Mtwara.

Pili, makubaliano yamefikwa juu ya kuunganisha miundombinu ya kusafirisha gesi asilia toka kwenye bomba kubwa la gesi kwenda kwenye kiwanda cha Dangote pamoja na kukamilisha mkataba wa awali (Gas Supply Term Sheet) kwa ajili ya mauziano ya gesi kwa matumizi ya kiwanda hicho.

Makubaliano haya yamefikwa ikiwa ni utekelezaji wa agizo la Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dr. John Pombe Magufuli akielekeza TPDC kukamilisha Makubaliano na Dangote juu ya mauziano ya gesi asilia ndani ya siku nne (4).

Kazi ya kuunganisha miundombinu ya gesi asilia kwenye mitambo ya kufua umeme utakaotumiwa na kiwanda hicho itaanza mara moja.

Imetolewa na:

Mkurugenzi Mtendaji,

Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania.

“TPDC kwa Maendeleo ya Taifa”